

MSAADAA WA KIFEDHA HABARI KWA WAZAZI

Kila mtoto wa Victoria anapaswa kupata ulimwengu wenye fursa za kujifunza ambazo zipo zaidi ya kuwa darasani. Msaada wa kwenda Kambi, Michezo na Matembezi husaidia kuhakikisha kuwa hakuna mwanafunzi atakayekosa fursa ya kuungana na wanafunzi wenzao kwa shughuli muhimu, za kielimu na za kufurahisha. Ni sehemu ya kufanya Victoria kuwa Mkoa wa Elimu na ahadi ya Serikali ya kuvunja kiunganishi katika asili ya mwanafunzi na matokeo yake ya kielimu.

MSAADAA WA KAMBI, MICHEZO & MATEMBEZI (CSEF)

Kambi za shule zinawapa watoto uzoefu mzuri wa kuhamasisha mazingira ya nje, matembezi huhamasisha uelewa wa kina juu ya jinsi ulimwengu unavyofanya kazi na michezo kufundisha kazi ya pamoja, nidhamu na uongozi. Zote ni sehemu ya mtaala mzuri

CSEF inatolewa na Serikali ya Victoria kusaidia familia zinazostahiki kulipia gharama za safari za shule, kambi na shughuli za michezo.

Ikiwa unashikilia kadi halali ya makubaliano ya punguzo au ni mzazi wa malezi ya muda mfupi, unaweza kustahiki CSEF. Kitengo maalum pia kipo kwa wanaotafuta hifadhi na familia za wakimbizi. Msaada hulipwa kwenye shule kutumia kwenye gharama zinazohusiana na kambi, safari au shughuli za michezo kwa faida ya mtoto wako..

Kiasi cha mwaka cha CSEF kwa mwanafunzi ni:

- \$125 kwa wanafunzi wa shule ya msingi
- \$225 kwa wanafunzi wa sekondari

HABARI ZAIDI

Kwa habari Zaidi kuhusu CSEF tembelea
www.education.vic.gov.au/csef

JINSI YA KUOMBA

Waombaji wapya wanatakiwa kuwasilaiana na ofisi ya shule ili kupata fomu ya maombi ya CSEF au kupakua kutoka www.education.vic.gov.au/csef

Ikiwa uliomba CSEF katika shule ya mtoto wako mnamo 2019, hauitaji kujaza fomu ya maombi mnamo 2020 isipokuwa kumekuwa na mabadiliko katika hali ya familia yako.

Unahitaji tu kujaza fomu ya maombi ikiwa kuna mabadiliko yoyote yafuatayo yamefanyika:

- **uandikishaji mpya wa wanafunzi;** mtoto wako ameanza au amebadilisha shule mnamo 2020 au haukuomba mnamo 2019.
- **Mabadiliko ya hali ya kifamilia;** kama vile mabadiliko ya utunzaji, mabadiliko ya jina, nambari ya kadi ya makubaliano, au ndugu zako wapya wanaoanza shulenii mnamo 2020.

Wasiliana na ofisi ya shule kama huna uhakika.

